**Haki ya Kuzungumza (Right to Speak)**
**0800 221 038 au wpp.ethicspoint.com au wppmobile.ethicspoint.com**

Hapa WPP, tumejitoa kuhakikisha kwamba kila mtu anafahamu na yuko huru kutoa na kuwasilisha maoni yake.

Hiyo ndiyo sababu tunatoa namba ya simu ya msaada isiyolipishwa na ya siri - Haki ya Kuzungumza , kwa wafanyakazi, wafanyakazi huru, washauri, wasambazaji na wahusika wengine kuripoti kuhusu maoni juu ya maswala ya biashara au tabia hapa WPP au kampuni zake za uendeshaji.

Hii ni huduma inayoendeshwa kwa kujitegemea inayolinda siri ya mtu yeyote ambaye asingependa kutambulika.

**Ninawezaje kuripoti taarifa kupitia Haki ya Kuzungumza?**
Matumizi ya namba ya simu ya Haki ya Kuzungumza ni ya hiari na ni ya siri kabisa. Huduma hii inapatikana saa 24 kila siku kwa: 0800 221 038 au wpp.ethicspoint.com au wppmobile.ethicspoint.com

Kwa urahisi kupitia simu ya mkononi, unaweza kusanikisha msimbo wa QR ulio hapa chini:

Namba ya simu ya Haki ya Kuzungumza inasimamiwa na NAVEX Global EthicsPoint, shirika ambalo si sehemu ya WPP,  kwa usaidizi duniani kote na katika lugha nyingi.

Ungependelea kuwasilisha wasiwasi wako mtandaoni, basi unaweza kufanya hivyo kupitia kiunganishi hiki: wpp.ethicspoint.com

WPP haivumilii tabia yoyote ya kulipiza kisasi dhidi ya watu wanaoripoti kuhusu Wasiwasi, Tumejitoa kutoa njia salama na ya siri kwa watu walio na wasiwasi wa kweli kuuwasilisha, na kufanya hivyo bila hofu ya kisasi.

**Tafadhali kumbuka:**
- Ukichagua kuwasilisha wasiwasi wako kupitia simu, basi tafadhali fahamu kuwa simu yenyewe haitarekodiwa
- Unapowasilisha ripoti yako utapewa chaguo la kutojitambulisha ukipenda.

**Je? nini hufanyika baada ya kuwasilisha wasiwasi au suala langu?**

- Mara baada ya ripoti kuwasilishwa, itasimbwa na NAVEX Global na kushirikiwa kwa usalama na Mshauri Mkuu wa Kundi la WPP na Mshauri Mkuu wa Hatari kwa Shirika ili kufanyiwa tathmini na uchunguzi kupitia kipengele cha Uadilifu wa Biashara cha WPP.
- Unaweza kusasisha ripoti yako kwa kuweka habari mpya wakati wowote kwa kuingia kwenye jukwaa la NAVEX Global EthicsPoint kupitia njia unayopendelea. Unaweza pia kutazama hali ya ripoti yako kupitia jukwaa la NAVEX Global EthicsPoint.

Kanuni za Maadili za WPP zinaweza kupatikana hapa:
http://www.wpp.com/wpp/about/howwebehave/governance/